

Mwenendo wa Kichumi na Ustawi wa Wanawake katika eneo la Madini ya Tanzanite Mirerani, Manyara

Civic Social Protection Foundation (CSP)
Septemba 2025

Muhtasari

Eneo la uchimbaji wa Tanzanite la Mirerani, lililoko kaskazini mwa Tanzania, ambalo ndio chanzo pekee duniani cha madini ya Tanzanite, lina umuhimu mkubwa wa kiuchumi kwa taifa na jamii zinazolizunguka. Hata hivyo, pamoja na fursa hii ya kipekee, sekta hii bado inakabiliwa na changamoto za kimfumo zinazoshabihiana na zile za sekta ya uchimbaji mdogo na wa kati. Wanawake wachimbaji wanakumbwa zaidi na changamoto hizo, hasa kupitia ubaguzi wa kijamii na kiuchumi unaowatenga na kuwanyima fursa za kunufaika ipasavyo na shughuli za uchimbaji. Utafiti huu unachunguza changamoto za kijamii, kiuchumi na kiafya zinazowakumba wanawake wachimbaji wa Tanzanite katika eneo la Mirerani, huku ukilenga kutoa maarifa ya kisera yatakasaidia kuboresha ustawi wao, uwezo wa kiuchumi, na kuwawezesha zaidi katika mfumo wa uzalishaji wa madini.

Utafiti umeongozwa na maswali matatu makuu: Ni changamoto zipi kuu za kijamii, kiuchumi na kiafya zinazowakumba wanawake wachimbaji wa Mirerani? Changamoto hizi zinaathiri vipi maisha na fursa zao za kujikwamua kiuchumi? Na ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa ili kupunguza pengo la kijinsia na kuboresha hali ya wanawake wachimbaji? Matokeo yanaonesha kuwa wanawake wengi wamesukumwa katika nafasi zisizo rasmi na zenye malipo duni kama kuchambua mawe ya madini, kubeba mizigo, kuuza chakula na kutoa huduma za usaidizi migodini. Wengi wao wanakosa fursa ya kupata mikopo, vifaa vya uchimbaji, na mafunzo ya kitaalamu, jambo linalowazuia kupiga hatua katika mnyororo wa thamani wa madini. Aidha, wanawake hawa wanakumbwa na changamoto nyingi za kiafya ikiwemo maumivu ya mwili, matatizo ya kupumua na msongo wa mawazo kutokana na mazingira duni ya kazi, ukosefu wa vifaa vya kujikinga, na huduma duni za afya.

Utafiti pia umebaini uwepo mkubwa wa wanawake wajane katika eneo la uchimbaji, wengi wao wakibeba jukumu la kulea familia pekee baada ya waume zao kufariki kutokana na ajali au maradhi yanayohusiana na uchimbaji wa madini. Hali hii inaongeza hatari ya kuendelea kuishi katika umaskini wa muda mrefu. Pamoja na hayo, wanawake hawa wameendelea kuonyesha ustahimilivu mkubwa kwa kutegemea vikundi vya akiba visivyo rasmi, msaada wa familia, na biashara mbadala kama njia ya kujikimu. Hata hivyo, mbinu hizi bado hazitoshi kuvunja vikwazo vya kimfumo wanavyokutana navyo. Kama alivyosema mchimbaji mmoja: “Wanaume ndio wanaingia kwenye migodi mikubwa yenye fedha nyingi. Sisi tunabaki na kazi ndogo – kuchambua mawe, kuuza chakula, au kusaidia tu. Hakuna anayetosomesha au kutupa vifaa vya kazi.”

Ingawa kuna juhudi kutoka kwa mashirika ya kiraia, viongozi wa jamii na serikali katika kusaidia wanawake wachimbaji, msaada huo mara nyingi huwa ni wa vipande vipande na usio na mtazamo wa kijinsia. Takribani theluthi moja ya wanawake waliohojiwa waliripoti kutopokea msaada wowote wa maana kutoka kwa wadau. Ili kubadilisha hali hii, hatua madhubuti zinahitajika, si kwa nia ya kuimarisha usawa wa kijinsia pekee, bali pia kuchochea ukuaji wa uchumi na ustahimilivu wa jamii kwa ujumla. Utafiti unapendekeza maboresho ya sera na vitendo kwa lengo la kuboresha mazingira ya kazi na maisha ya wanawake wachimbaji, ikiwa ni pamoja na: kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kupitia mikopo midogo yenye masharti rafiki kwa wanawake; kuimarisha usalama na afya kazini kwa kudhibiti matumizi ya vifaa vya kujikinga na mazingira bora ya kazi; kupanua fursa za mafunzo na ujuzi wa kiuchimbaji kwa wanawake; na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa kuanzisha vituo vya afya vya muda (kliniki tembezi).

Kwa kuchukua hatua hizi, watunga sera, kampuni za madini, mashirika ya kiraia na viongozi wa jamii wanaweza kujenga sekta ya uchimbaji wa Tanzanite iliyo jumuishii, yenye usawa na endelevu, inayowezesha wanawake wachimbaji kushiriki kikamilifu na kunufaika na rasilimali hii muhimu kwa maendeleo ya kanda.